GILASI YA MWISHO MAKABURINI- SAID A MOHAMED MANDHARI NA WAKATI

Hii ni hadithi inayolenga mazingira ya mjini. Kuna bendi mbalimbali ambazo zinaburudisha waja. Muziki wa Michael Jackson unadhihirisha wakati ambapo muziki wa kimagharibi ulikuwa ukienziwa na wengi katika vyumba vya starehe. Mwandishi tunakisia alilenga wakati wa miaka ya sabini na themanini enzi ya imani za kishirikina.

Anwani

1. Baada ya msoi na wenzake kula, kunywa na kumaliza na vyombo vya vyakula kuondolewa zilibakia chupa za gilasi za vinywaji (Gilasi ya mwisho makaburini)
2. Gilasi zilianguka na kuvunjika baada ya ukemi kupigwa na watu wakaanza kukimbilia maisha yao.
3. Baada ya majambazi /vizuu kuwavamia watu, wengi labda hawakuwahi kurudi huko
4. Wakati majambazi walivamia, starehe, ulevi na disko ilikuwa imefikia kilele.

Dhamira

i) Mwandishi anatueleza ya kuwa ni vizuri tuepukane na imani au itikadi potovu ambazo zinaweza kutuletea madhara kama vile kukosa raha na imani katika maisha yetu. Anatuambia tuepukane na ushirikina.

ii) Mwandishi anatuonyesha namna baadhi ya watu walivyokataa kubadilika na wakati. Msoi ni kielelezo chema cha mtu ambaye bado hajazinduka.

iii) Mwandishi anatuonyesha aina mbalimbali za starehe za watu mkahawa huu wa Exotic Resort ni wa wale tu walio na nguvu ya kifedha na nafasi katika jamii.

iv) Mwandishi anawaasa wanajamii kuwa na msimamo katika maamuzi yao. Kutokana na kukosa msimamo Msoi anapata madhara ya kuvamiwa na majambazi.

Maudhui

i) Imani na itikadi za ushirikina
ii) Starehe na Anasa
iii) Uhalifu /ujambazi
iv) Utabiri na ndoto
v) Urafiki
vi) Msimamo

a) Imani na itikadi za ushirikina

1. Maudhui ya ushirikina yametawala hadithi nzima Msoi aliota ndoto za kishirikina na kuziamini. Wakati mwingine aliota ndoto akiwa macho UK 32. Ndoto hizi zilimpa uwezo wa kutabiri mambo. Aliota kuwa mahali

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

walipokwenda na marafiki zake kupitisha wikendi hapakuwa pa wanadamu hai bali pa wafu. Aliamini ushirikina huu na hata akatishia kukataa kwenda katika baa ya makaburini. Hata ingawa Semkwa alifaulu kumshawishi kwenda, alienda shingo upande.

2. Ushirikina pia unajitokeza wakati anapojikwaa mlangoni na bakuli lake la maua likavunjika vipandevipande. Kwake hiyo ilikuwa ishara mbaya iliyomtahadharisha dhidi ya mabaya ambayo yangetokea mbeleni.
3. Baada ya kuvunjika kwa bakuli lake la maua, mguu wake wa kushoto ulikosea mizani, akapepesuka na kutaka kuanguka kutokana na ushirikina aliamini pia kuwa ni onyo.
4. Msoi alijibana kidole kidogo akatoa usiyahi alipokuwa akifunga mlango wa gari. Semkwa alikuwa akiyafuatilia matukio hayo yote, anasema "una nini Msoi leo? Ama kweli itikadi na ushirikina vimekudhibiti kewli kweli.
5. Njiani walipokuwa wakielekea kwenye baa ya makaburini hali ya anga ilibadilika ghafla, kukawa na radi iliyopasua mbingu na mngurumo. Haya yote hayakusababisha kunyesha kwa mvua. Msimulizi anasema "kwa Msoi hiyo ilikuwa ishara mbaya".
6. Kwenye baa ya makaburini, Asha anamchokoza Msoi kutokana na hali yake ya kuamini katika ushirikina. Anasema, " leo Msoi umebadilisha makao? Umeona ukalie kiti kitakachokupa mandhari ya mava? Kwani ndiko yatakakozuka mazingaombwe unayoyatabiri?
7. Asha alipotazama juu angani na kuona nyota alisema, " Tazama, hata mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu leo. Hizi ni imani za kishirikina.
8. Josefina pia aliamini katika ushirikina. Anasema, "Bwana huyu akishikia lake kama ziraili, mpaka aitoe roho ya kiumbe" Imani za kishirikina zinazojitokeza hapa ambapo Josefina anaposema kuhusu ziraili. Ziraili anaaminika kuwa ni malaika wa mauti ambaye huleta vifo katika jamii kundi la vizuu lilipoonekana kwenye mava watu wote walipiga ukemi walikimbilia usalama wao. Msimulizi anasema, ".....ukafuatiwa na kwenzi na kwenzi zikiwa mjumuiko wa zogo na ghasia. "(UK37) watu hawa waliamini katika ushirikina ndipo haya yakatokezea.

b) Starehe na anasa

1. Watu kama vile Msoi, Josefina na Asha pamoja na watu wengine walikuwa na mazoea ya kutembelea vilabu kama baa ya makaburini kila wikendi kustarehe.
2. Kulikuwa na unywaji vileo mbalimbali na vyakula vya kila aina ulevi uliamsha jadhba ya washirika.
3. Kuna burudani ya miziki mbalimbali. Bendi na mziki wa Michael Jackson unaporomoshwa pale.
4. Jina la baa hii makaburini linaonyesha kuwa mahali hapo palikuwa na mapepo fulani yaliyowapagawa watu.
5. Watu walivalia mavazi mbalimbali na kujipaka marashi ya kila aina.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

6. Mahali pale palikuwa kama peponi. Duniani ni ahera mahali pa starehe kwelikweli, hata Msoi alienda ingawa alikuwa ana utabiri wa jambo baya kutokea.
7. Kupitia kwa vyombo vya habari tunaelezwa kuwa baa hii ni 'exotic resort' ya kifahari "pahala wanapozuru wangwana kama wao wenye vyao.
8. Sehemu kama hizo za starehe za usiku huenda si pahali pa usalama kwa kuwa zogo huweza kuzuka na watu wakaumizana au kuumizwa.

c) Uhalifu /ujambazi

1) Ilitangazwa katika runinga kuwa majambazi waliojifanya vizuu mavani waliibia baa ya makaburini kila kitu pamoja na wateja wao.
2) Miji au majumba ya starehe kuna visanga au visa vya ujambazi ambavyo huweza kushuhudiwa.
3) Visa vya ujambazi huwatia watu hofu na kusababisha fujo au ghasia kwa wapenda amani K.M. ujambazi huo katika baa ya makaburini ulisababisha mtafaruku; meza kuanguka, viti kuvunjika, gilasi na sahani kuvunjika nazo taa zikazima.
4) Wateja kama vile Semkwa na Josefina waliibiwa pesa, nguo, viatu na hata chupi.
5) Majambazi walefu na sugu waliovalia kama vizuu ili kuwatisha watu pale kwenye baa na kuwaibia kwa urahisi.
6) Msoi na Asha walibahatika kutoroka lakini walilazimika kukimbia mwendo mrefu kufika nyumbani (uoga ulifanya wasahau gari).
7) Majangili walivalia kama vizuu na walinuka kama maiti - kutisha.

d) Utabiri/ndoto

1) Msoi ni mtabiri wa mambo ambayo yatatokea kabla yatokee.
2) Kuna ishara zinazotangulia ndoto hizi kama malaika kusimama mwilini na mwili kutetemeka.
3) Kuna dalili ambazo hutangulia tukio baya kama aliligonga bakuli la maua ambalo lilivunjika, karibu aanguke na mlango wa gari ulimbana mkono. Hali ya anga ilibadilika kukawa na wingu jeusi.
4) Watu wengi hasa vijana katika karne hii (Semkwa, Asha na Josefina) hawakuamini katika maono (utabiri) yake. Waliamini yalitokea kisadfa tu.
5) Ndoto ya Msoi ya vizuu ilikuja kuwa halisi wakati wimbo wa Michael Jackson wa Thriller ulipokuwa unaimba.

e) Urafiki

1) Marafiki wamekuwa wakienda katika baa ya makaburini kila Jumamosi.
2) Wanaoenda huko huwa ni watu wenye mahusiano na mielekeo inayofanana. K.M. Semkwa alipogundua kuwa mwenzake haonekani hotelini, anaamua kuenda kumtafuta kwake. Huu ni uhusiano wa kujuliana.
3) Asha na Josefina walikuwa wakiwangojea rafiki zao kuwasili huko hotelini.
4) Kama marafiki walioshibana, wanatumbuizana na kuzungumza kama njia ya kuuimarisha uhusiano wao.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

5) Kabla ya Msoi kufika hakuna kilichoagizwa pale hotelini, huenda ikawa walikuwa wanangojeana.
6) Urafiki wao unadhihirika wakati Msoi na Asha wanapojinusuru na kujaribu kuwapigia simu Semkwa na Josefina. Hatimaye Semkwa anampigia simu Msoi kumweleza walikuwa salama.

f) Msimamo

1) Msoi hakuwa na msimamo
2) Zaidi ya kuhisi kuna hatari mbele yake na kudhamiria kutoenda tena katika baa ya mavani, bado anakubali kwenda kutokana na kushauriwa na Semkwa.
3) Matokeo yake anapata madhara ya kuvamiwa na majambazi na kuporwa vitu kama angekuwa na msimamo thabiti asingefikwa na hayo
4) Hapo tunaona nafasi ya marafiki katika kutupotosha. Marafiki wa Msoi ndio wanaompotosha na kumshawishi kwenda baa ya mavani hali akiwa hataki.

WAHUSIKA

MSOI

1) Rafiki wa dhati
   Walipokuwa nyumbani walijaribu kuwapigia simu za mkononi Asha na Josefina ambao ni marafiki.
2) Mshirikina
   Aliamini katika ndoto na ishara katika maisha yake ambazo zilimpa utabiri wa yajayo kila mara
3) Mpenda raha
   Alienda kila wikendi kwenye baa ya makaburini
4) Mwenye bidii
   Alifanya kazi wiki nzima kabla ya kuenda kwenye baa ya makaburini
5) Mwoga
   Anaogopa vizuu; akatimua mbio bila kusita baada ya kuviona vizuu, alisahau gari lake na marafiki zake
6) Ana imani
   Mradi ameoteshwa, aliona lazima jambo hilo litokee. Wakati mwingine alikosa kuwa makini kwa sababu alitarajia jambo hilo kutokea.
7) Hana msimamo thabiti /kigeugeu
   Anashawishika haraka anashawishika kwenda baa ya makaburini licha ya kuwa alikuwa amehisi hatari iliyo kuwa mbele yake.
8) Mwenye hasira
   Anapofanyiwa mzaha na wenzake kama Asha anakasirika haraka. Alitaka wamwamini bila maswali mengi.
9) Mwenye uwezo wa kutabiri
   Alikuwa na uwezo wa kutabiri mambo ambaye mara nyingi yalitokea. Alitabiri kutokea kwa jambo baya katika baa ya makaburini ingawa hakufahamu jambo lenyewe, inatokea kwamba baa hiyo inavamiwa na wezi waliojifanya kuwa mizuka.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

10) Mcheshi/mwenye mzaha

Baada ya utabiri wake kutokea, anafanyia wenzake mzaha kwa kuwaambia kwamba waliwakimbia kwa sababu iliwabidi wajinusuru na wale vizuu hata baada ya kufahamu walikuwa majambazi.

11) Mwenye pesa

Baa ya Exotic Resort ilikuwa ghali sana ambayo ilihudhuriwa na wenye pesa, pia alikuwa mwenye gari.

12) Mchezaji dansi hodari

Alicheza dansi hadi kuonekana kana hana mifupa

13) Mkakamafu

Yeye na Asha walikimbia kwa muda wa saa moja na nusu hadi kwake.

Umuhimu wake

a) Anaendeleza maudhui ya ushirikina- anaota na kutabiri wizi katika baa ya makaburini. Aliamini wafu wangefufuka na kuwafukuza pale.
b) Anaonyesha ubadhirifu utumizi wa pesa ovyo kwa ulevi na starehe kila wikendi akiandamana na wenzake.
c) Anaendeleza uoga-kutimua mbio ajabu na kuacha gari na wenzake nyuma. Aliwapigia Semkwa na Josefina simu baada ya kufika salama.
d) Kielelezo cha usasa ulioathiriwa na imani za kikale za kishirikina.
e) Kupitia kwake mwandishi ameonyesha jinsi imani za kishirikina zinavyoweza kuyatawala maisha ya mtu hata kuathiri wanaohusiana naye.

Semkwa

Rafikiye Msoi

a) Mpenda anasa na starehe

Tunamuona akimshinikiza Msoi waende katika baa ya makaburini. Alimkumbusha kuhusu marafiki wao wa kike Asha na Josefina ambao waliwasubiri klabuni.

b) Mwenye utani/mzaha.

Katika mazungumzo yake na Msoi na marafiki zao Asha na Josefina alionekana akizunguza kwa utani mwingi sana.

c) Kijana asiria /kijana wa kisasa.

Anasema imani na itikadi haistahili kutawala maisha yao, wao wanaishi na kuongozwa na sayansi.

d) Mwenye kejeli

Anamwambia Msoi eti una nini Msoi? Ama kweli itikadi na ushirikina vimekudhibiti kwelikweli.

e) Ana uwezo wa kushawishi

Kutokana na ulimi mzuri, anamshawishi Msoi kuandamana nao hotelini

f) Jasiri

Baada ya 'mizuka' kujitokeza makaburini usiku huo, yeye hakutoroka, kumbe walikuwa majambazi wakapora wateja yeye akiwemo.

g) Mbadhirifu

Kutumia pesa katika starehe kila wikendi.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

Umuhimu

a) Anaendeleza maudhui ya starehe na anasa kutembelea vilabu usiku na kujivinjari na kulewa huku ameandamana na wasichana kama Josefina.
b) Itikadi /ushirikina-anapuzilia mbali utabiri wa Msoi hata baada ya kuporwa hakuamini ni mizuka.
c) Raha-anafurahia ujana na kuonyesha jinsi vijana wengi wanafurahia maisha ya anasa
d) Kielelezo cha urafiki wa dhati

Asha

a) Mpenda anasa
   Msichana anayependa anasa na kuandamana na vijana wa kiume kama Msoi kwenda katika baa ya makaburini exotic resort
b) Mwoga
   Alitimua mbio na kukimbilia usalama alipoona vizuu, alimfuata Msoi
c) Kijana wa kisasa
   Hakutaka kuamini yale anayoambiwa na Msoi juu ya ushirikina na utabiri wake
d) Mchangamfu
   Anapenda kushiriki maongezi yenye mizaha na wenzake alipomwona Msoi amekaa kwenye makao mbayo si ya mazoea yake anamwambia, " leo Msoi umebadilisha mkao
e) Mwenye mzaha
   Anamtania Msoi ambaye ana wasiwasi katika eneo la burudani. Anamwambia, " leo Msoi umebadilisha mkao? Umeona ukalie kiti kitakachokupa mandhari ya mava? Kwani ndiko yatakakozuka mazingaombwe unayotabiri?
f) Jasiri
   Hata baada ya Msoi kutabiri kwamba jambo baya litatokea katika eneo lao la starehe, anaandamana na Josefina kwenda kule. Anasema kwamba hawatatoka pale.

UMUHIMU

Anawakilisha wanawake ambao wanaenzi burudani maishani. Kupitia kwake mwandishi anatubainishia imani za Msoi.

JOSEFINA

a) Mnyamavu-hapendi kushiriki maongezi sana
b) Kijana wa kisasa- haamini nguvu na maono ya ushirikina kama ulivyoendelezwa na Msoi
c) Anapenda anasa- alikuwa miongoni mwa wale waliofika mapema huko baa ya makaburini siku hiyo ya Jumamosi.
d) Jasiri- hakutimua mbio kama Msoi na Asha. Alibaki pale na Semkwa na kuporwa na wale majambazi.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

UMUHIMU

Anaonyesha jinzi wasichana wa kisasa wanavyovinjari katika vilabu usiku. Hakuamini maneno ya Msoi kuhusiana na ushirikina.

MAJAMBAZI

a) Wajanja- kuvalia vizuu na kuwapora wateja wa baa ya makaburini. Mavazi haya yalizua taharuki na kuwafanya wengi kuchanganyikiwa na wengine kama Msoi kutoroka na kuacha gari lake.
b) Wakatili
   Kuwapora wateja kila kitu na kuwaacha uchi wa mnyama hawakujali aibu waliyowaacha.

UMUHIMU

a) Wanaendeleza maudhui ya wizi / uhalifu ujambazi walitumia nafasi yao kwa kuvalia vizuu kwa sababu baa inaitwa makaburini. Wanatokea wakati ule tu wimbo wa Michael Jackson wa Thriller ulipokuwa unaimba
b) Wanaendeleza uozo wa kijamii- wanawapora watu mali yao yote na kuwaacha uchi majambazi hawataki kufanya kazi halali.

WATEJA NA WAHUDUMU WA MAKABURINI BAA

a) Wanapenda starehe
   Wanashiriki katika vileo, vyakule na mziki kila wikendikwenye baa ya makaburini na wateja wengi sana
b) Itikadi na ushirikina
   Wengine waliamini ni vizuu na kutoa habari hizo kwa polisi ilhali wengine waliamini ni majambazi na kutoa habari hizo kwa polisi, habari katika vyombo vya utangazaji zilikuwa za kutatanisha.
c) Wahudumu nia yao ni kupata pesa. Baa hii ni kitega uchumi

UMUHIMU

a) Wanaendeleza maudhui ya starehe na anasa wanapofika hapo na kuwahudhuria wateja usiku.
b) Wengine waliamini itikadi na ushirikina ilhali wengine waliona ni hali ya kawaida ya ujambazi.

MBINU ZA LUGHA

TASHBIHI

a) Kusimama kama kijiti UK 32
b) Hisia hiyo kali ilikuwa imeumuka haraka kama hamuri lililojazwa hamira UK32
c) Umebaki kulala kochini kama mgonjwa wa malaria UK33
d) Utabakije juu ya kochi kama mgonjwa wa homa na leo ni Jumamosi? Uk33
e) Alijua ni kitu kama jabali lenye mshindo mkuu uk33
f) Anatutisha sisi kama watoto wadogo, anatutisha kaka uk35
g) Bwana huyu…kama ziraili, mpaka aitoe roho ya kiumbe uk35
h) Na wewe, mpaka unigande mimi tu kama kupe?
i) Mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamo wa mto uk 37
j) Kung'ang'anaa kama masanamu uk 37-38

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

TASHIHISI

Vitu visivyo na uhai kupewa uwezo wa kutenda kama vitu vilivyo na uhai ili kusisitiza hali na pia kumvutia msomaji.

a) Wafu wenyewe wakiwa mapumzikoni wamechoka kukerwa, na kwa hivyo siku yoyote ile wangefanya kitu kujihami uk32 kauli hii imetumiwa kulainisha hisia za kishirikina za Msoi.
b) Imani yako imekutawala uk 33. Imani imepewa uwezo wa kutawala, kauli inayosisitiza jinsi imani yake Msoi inavyomwathiri.
c) Hutaki kuiacha ijapokuwa unajua kwamba haina haki ya kuketi wala kusimama katika maisha yetu ya sasa(uk33) kauli hii ya Semkwa inahuisha imani ili kusisitiza kuwa imani za kishirikina hazifai.
d) Njiani, mbingu ghafla ilikasirika-ikafunga uso wake mweusi (uk34) mbingu kutandazwa na Mungu.
e) Mbingu ilifanya hivyo, mara moja tu, tena bila ya kutiririsha hata tone moja la chozi.
f) Hata mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu leo.
g) Harufu za mafuta mazuri ghali na ya fahari, zilikuwa zimekazana kuzikalia juu harufu za vyakula.
h) Kinywaji kilipotua juu ya meza tu, jamaa walinyanyua gilasi zao.
i) Hali ya hewa ilikuwa nzuri, baada ya kutishwa kuharibiwa na ile radi.
j) Msoi alipozitazama taa siku hiyo, zilikuwa na mwako wa huzuni.
k) Jimwili jeusi la usiku
l) Hakucheza mpaka muziki ukamwingia damuni.

UTOHOZI

a) Wikendi-weekend
b) Kochini- coach
c) Sofa- sofa set
d) Baa- bar
e) Swichi-switch
f) Kauntani- counter
g) Bendi- band
h) Muziki- music
i) Gilasi – glass
j) Stimu- steam

TASWIRA

a) Maelezo ya mwandishi kuhusu baa ya makaburini
b) Picha ya baa ya makaburini ilikuwa machoni mwa Msoi
c) Maelezo ya jinsi hali ya anga ilibadilika punde Msoi na Semkwa walipotoka kuelekea mahali pao pa starehe (wingu jeusi)
d) Maelezo ya jinsi wateja walivyojistalehesha kule kwenye baa.
e) Picha ya watu wakitoroka walipoona vizuu. Wengine kustaajabu hata kushidwa kutoroka

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

f) Mavamizi ya majambazi waliojifanya vizuu mavani
g) Msoi na Asha walivyokimbia kutoka baa ya makaburini.

TAHARUKI

a) Hadithi nzima ni taharuki kuanzia ndoto na utabiri wa Msoi, mikosi ambayo inamkumba kabla hawajaondoka ni dalili mbaya. Wasiwasi mwingi na kisha vizuu kutokea. Mahali penyewe kuitwa makaburini kuanzia mwanzo msomaji anaandaliwa juu ya wizi hapo mwisho.
b) Namna ambavyo watumishi walikimbia huku na huku, mara vinywaji, mara chakula.
c) Matatizo na ghasia zilizozuka huko baa ya makaburini na matokeo.
d) Msoi alikuwa katumbua macho yake mpaka yale macho yakaonekana kama yanataka kudondoka chini kutoka vibakuli vyao.kisha, taratibu Msoi alimpelekea mkono wa kushoto…
e) Baada ya kuvamiwa na majambazi waliojifanya vizuu, baa ya mavani iliendelea na umaarufu wake au la;
f) Baada ya kisa hiki msimamo wa Semkwa, Josefina Asha na Msoi utakuwa upi?

TAKRIRI

a) Rejea tena, piga tena…… muziki anza tena rejea tena
b) Raha, raha, raha inamfunika kila mtu
c) Ndoto zake za ajabu ajabu
d) Inuka, inuka bwana
e) Anatutisha kaka, anatutisha sizi kama watoto wadogo, anatutisha kaka.
f) Utapigwa tena na tena
g) Duru kwa duru
h) Furaha, furaha, furaha imechanua

NDOTO /UTABIRI

a) Ndoto zinaendeleza ushirikina
b) Wakati aliota, ndoto inamwonyesha kuwa mahali pale wanastarehe kila wikendi (baa ya makaburini) si pazuri.
c) Msoi anaota ndoto ambazo hubashiri yale yatakuja kutokea
d) Ndoto hizi huambatana na matukio ambayo anakuja kuamini ni onyo k.m wingu jeusi, kuteleza karibu aanguke n.k
e) Ndoto hii ilikuja kutokea
f) Ndoto hii ilimfanya awe macho, kwa hivyo aliweza kutoroka na hakuporwa.

KINAYA

a) Wakati muziki wa Michael Jackson unaimbwa majambazi wanafika wakiwa wamevalia kama vizuu.
b) Wateja walijipaka mafuta na manukato yaliyonukia vizuu walijipaka uvundo ulionuka kama maiti.
c) Taswira ya makaburini ni ya kinaya pahali patulivu panavutia, ladha tamu, aali, penye upekee wa mvuto wa mazingira ilhali panapakana na makaburini.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

SITIARIA

a) Maji ni kinywaji cha uhai
b) Kinywaji ni petrol ya muziki

CHUKU

a) Vinywaji vyake vya kuburundisha na kupoza joto la wiki nzima
b) Hali ya u-exotic unaompa mtu kujihisi yumo ndani ya starehe nje ya dunia halisi ya wiki nzima isiyokwisha mahangaiko na mashughuliko.

SEMI

a) Kupitisha wikendi – kustarehe
b) Kitu kinacholizia ndege mbaya – Mkosi
c) Kung'oa nanga – ondoka
d) Yaingie sura – kubadilika
e) Kukondoa macho – shangaa
f) Moyo mzito- mwenye huzuni
g) Shingo upande – bila kupenda
h) Uso kwa uso – onana macho kwa macho

MASWALI YA BALAGHA UK 34-35

a) He, saa mbili na nusu hujajitayarisha?
b) Ah ndio huendi?
c) Yaani umegoma?
d) Imani yako imekutawala vilivile, au siyo?
e) Una nini Msoi leo?
f) Radi ngapi zimepiga tokeo dunia kuumbwa?
g) Mimweso ningapi imemeta tokea mbingu kutandazwa na Muumba?
h) Kipi cha ajabu kitachomfanya mtu awe na hofu?
i) Hofu hiyo itoke wapi katika usiku huu mwema uliojaa furaha na utukutu wa ujana?

ISHARA

a) Ndoto ni ishara ya yaliyobanwa fikirani au yatakayotokea Msoi aliamini katika ndoto zake kiasi kwamba aliweza kuota mchana na akashindwa kulala usiku msimulizi anasema, " Akawa anaota ndoto mchana kutwa, na usiku akashindwa kulala" aliota kuwa mahali walipozoea kwenda yeye na marafiki zake kupitisha wikendi si pahali pa binadamu hai, ni pa wafu na wafu wenyewe wakiwa mapumzikoni wamechoka kukerwa, na kwa hivyo siku yoyote ile wangefanya kitu kujihami (uk 32) ndoto hii inatimia baadaye. Ilikuwa ishara ya shambulizi lililowapata. Msimulizi anasema, " kule mavani kundi la vizuu limejifufua kwa mtindo wa Thriller wa Michael Jackson (uk37)
b) Wasiwasi aliokuwa nao Msoi ulikuwa ishara ya maafa ambayo yangetokea wasiwasi huu ulimfanya awe na moyo mzito na aliinuka kwenda baa ya makaburini shingo upande. (uk 33)
c) Picha ya baa ya makaburini ilikuwa machoni mwa Msoi (uk33) akili yake ilishika kumtabiria kitu asichokijua ingawa alijua ni kitu kama jabali lenye mshindo mkuu

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

linapoanguka utabiri huu ni ishara inayokamilika wakati wa mavamizi wakiwa katika baa ya makaburini.

d) Msoi alijikwaa mlangoni na bakuli lake la maua likavunjika vipandevipande uk 34. Hii ilikuwa ishara kuwa safari ya baa ya makaburini itavunjika vipandevipande. Inatimia wakati watu wanashambuliwa na kila mtu kukimbilia usalama wake.
e) Msoi alipokuwa akiteremsha mguu wake, mguu wa kushoto ulikosea mizani, akapepesuka na kutaka kuanguka (uk 34) rafiki yake Semkwa alimshika mkono na kwa hivyo hakuanguka. Hii ilikuwa ishara mbaya ya siku hiyo. Inatimia wakati wanavamiwa na kuwa karibu kuangamizwa kwenye baa ya makaburini lakini mbio zao zinawaokoa.
f) Msoi alipoingia garini, alipokuwa akifunga mlango wa gari alijibana kidole kidogo, akatoa usiyahi (uk 34) hii ni ishara ya maumivu ambayo angeyapata. Ishara hii inatimia wakati anayahisi maumivu baada ya kutoroka shambulizi katika baa ya makaburini wakiwa na Asha.
g) Semkwa na Msoi walipokuwa njiani kuelekea baa ya makaburini hali ya anga ilibadilika ghafla, radi na ngurumo zikasikika. Hii ilikuwa ishara ya kuwatahadharisha kwamba maafa huenda yakatokea walipokuwa wakienda.
h) Kubadilisha mkao kwa Msoi akaketi akielekeza macho yako mavani ni ishara ya kuwa matukio yangetokea huko.
i) Taa kulingana na Msoi ziliwaka mwako wa huzuni kuashiria mabaya ambayo yangetokea uk35
j) Msoi hakucheza muziki kwa usogora wake wa kila siku, alicheza kwa kumwondosha mwenzake njiani tu kutokana na wasiwasi ulioshiria yale ambayo yangerokea.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

DAMU NYEUSI

Dhamira

1. Mwandishi anajaribu kuonyesha ubaguzi ambao hufanywa na wazungu dhidi ya watu weusi, wao hawahesabiwi kama binadamu kamili. Wazungu hawataki kabisa kutangamana na watu weusi.
2. Ubaguzi huu huwa mkali sana kiasi kuwa wamarekani wenyewe hubaguana kwa misingi ya rangi. Wamarekani weupe huwabagua wamarekani weusi.
3. Anadhamiria vilevile kuonyesha masaibu yanayowakumba waafrika ambao huenda Marekani wakitafuta kujiimarisha. Wao hudharauliwa, hubaguliwa, hutusiwa nk.
4. Anajaribu vilevile kuonyesha kuwa kuna tofauti kubwa sana ya kijamii kielimu na kiuchumi na hata kimazingira kati ya Marekani na Afrika Mashariki.
5. Kupitia kwa hadithi hii mwandishi vilevile anaonyesha matatizo yanayozikumba nchi za Afrika, mfano ulevi, uyatima, umaskini nk.
6. Pia anataka kuwasuta waafrika ambao wanataka kwenda ng'ambo wakifikiria kuwa maisha ni mazuri huko. Anawaonyesha masaibu mengi ambayo watapitia endapo wataenda kule.

MAUDHUI

Ubaguzi wa rangi

Wazungu wanawabagua waafrika na hata wamarekani wenzao kwa misingi ya rangi na maeneo watokamo ubaguzi wa rangi unajitokeza hivi.

1. Uk 23 – Fikirini anadharauliwa kwa kuwa yeye ni mwafrika tena mweusi. Anaulizwa maswali ya kudunishwa.
2. Uk 22 – dereva wa basi anakataa kusimama kwenye kituo cha mabasi na kumwacha Fikirini. Anakataa kusimama kwa kuwa Fikirini ni mweusi na dereva mwenyewe ni mweupe.
3. Uk 23 – Fikirini anatozwa faini na polisi mzungu kwa kuvuka barabara huku taa za kuelekeza magari zikiwa zimewaka rangi nyekundu.
4. Uk 24 – vyuoni alama hutolewa kwa kuwapendelea wanafunzi weupe na kuwakandamiza weusi.
5. Uk 24 – Fikirini aendapo kununua vitu kwenye maduka makubwa mlinzi humtafutatafuta kana kwamba anashuku atadokoa vitu vya watu.
6. Uk 24 – jela imeundiwa mtu mweusi. Wanaume weusi hawapati shahada vyuoni na badala yake wanang'ang'ania kula kalenda.
7. Uk 24 – anapoenda mkahawani anatazamwa kwa jicho la dharau na wateja na wahudumu.
8. Uk 24 – Fikirini anaposahau kufunga zipu anaitiwa polisi kuliko kukumbushwa tu aifunge. Inadaiwa kuwa amefanya hivyo maksudi ili kuonyesha uchi wake.
9. Uk 27 – Fiona na Bob wanamfanyia ukatili japo wao pia ni weusi kama yeye. Bob anatisha kumpiga risasi naye Fiona anatishia kumkata nyeti zake.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

10. Uk 27 – hata wazungu weusi wanawaona waafrika kama ambao wameenda huko kuwasumbua kuliko kukaa kwao Afrika.
11. Uk 27 – wazungu wanawaona waafrika kama tumbiri.
12. Uk 26 – wazungu wenyewe wanabaguana Fiona anamwambia Fikirini kuwa kwa watu weupe, kila mtu mweusi ni jambazi.

Elimu

1. Vijana kutoka Afrika mashariki hupata udhamini kusomea vyuo vikuu huko ng'ambo mf. Fikirini anaenda Marekani kupata shahada ya uzamifu katika kiingereza.
2. Wanafunzi wazungu wanawabagua wanafunzi weusi kwa kuwauliza maswali ya kijinga na ya kuudhi.
3. Wahadhiri wanatoa alama kulingana na rangi. Mwanafunzi mweupe anapata maki nyingi kuliko mwanafunzi mweusi.
4. Wamarekani weusi hufungwa jela na wanajipata wakitumikia kifungu kuliko kusoma.
5. Nchi za kiafrika zinahitajika kumarisha elimu ili wanafunzi wao wapate elimu papa hapa.
6. Wazungu hawaaamini kuwa waafrika wanaweza kumudu kiingereza. Ndio maana wanamwuliza Fikirini iwapo anajua kiingereza.
7. Licha ya kusoma elimu ya vitabu, Fikirini analazimika kusoma elimu nyingine inayohusu maisha ya ugaibuni, mfano namna ya kujibu maswali ya upuuzi amabayo anaulizwa na wazungu.
8. Pindi wanafunzi hawa wanapomaliza masomo yao wanafaa kurudi kwao ili kuiendeleza nchi yao. Fikirini anataka kumaliza masomo arudi nyumbani.

Uhalifu

1. Visa vya uhalifu ni vingi mno huko Marekani. Wamarekani weusi hujipata wakila kalenda kuliko kusoma. Hii ni kwa sababu wanashiriki sana katika visa vya utovu wa nidhamu.
2. Fiona anajifanya mhisani wake Fikirini lakini katika maisha halisi yeye ni jambazi na kahaba.
3. Chumba chao Fiona na Bob hutumika kama mahali pa kuwaibia na kuwanyanyasa watu hasa wageni. Fikirini ananyang'anywa pesa zake na vitabu.
4. Wahalifu wana silaha kali kama bunduki na visu. Bob anamtishia Fikirini kwa bunduki naye Fiona natishia kumkata nyeti kwa kisu.
5. Fikirini anavuliwa nguo na kulazimika kutembea uchi wa mnyama.

Upweke

1. Awapo ugenini, Fikirini anatamani vyakula vya nyumbani – ugali, matoke, mlenda, mihogo, wali na pilau.
2. Pia anatamani pombe za nyumbani kama waragi, gongo na chang'aa.
3. Upweke vile vile unamfanya Fikirini akumbuke wasichana wa kwao. Anasema kuwa wanapendeza na vile vile wana roho safi, wakilinganishwa na wale wa Marekani.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

4. Aibu ambazo alipitia zilimfanya atamani kumaliza masomo arudi kwao Afrika.

MASWALA IBUKA

1. Elimu – Fikirini anapata udhamini kwenda Marekani kusomea shahada ya uzamifu katika kiingereza. Afikapo huko anateswa na kubaguliwa. Nchi za kiafrika hazijaimarisha elimu vilivyo. Ndio maana watu weusi wanalazimika kutafuta masomo ya juu huko Marekani.
2. Ubaguzi wa rangi – wazungu hawapendi waafrika na huwaona kama wanaoenda huko kuwasumbua. Fikirini anabaguliwa kwa kuwa alikuwa mweusi.
3. Wizi/ujambazi – Fikirini anadanganywa na Fiona na kuingizwa nyumbani kwao. Anapokataa kulala na Fiona anaporwa kila kitu na kufurushwa nje uchi. Wamarekani weusi hujipata kifungoni kuliko vyuoni.
4. Hali ya anga/mazingira – kimazingira, ng'ambo ni tofauti na Afrika Mashariki. Uharibifu wa mazingira unasababisha ukame. Kinyume na Afrika Mashariki, ng'ambo kuna baridi kali na theluji. Inambidi Fikirini kuvaa nguo nyingi ili kupambana na baridi.
5. Pombe haramu - Fikirini anashiriki ulevi wa chang'aa, gongo na waragi akiwa Afrika Mashariki. Hivi ni vileo haramu.
6. Ukahaba – Fiona ni kahaba. Anafanya kitendo kile na wanaume kwa malipo. Ajabu ni kuwa haonekani kuwa na ada maalum anayotoza na inategemea makubaliano kati yake na mteja.
7. Unafiki – Fiona anajifanya rafikiye Fikirini kumbe ana nia ya kufanya ukahaba naye. Alimdanganya kuwa alitaka kumpeleka shuleni lakini alitaka kumwingiza kwa nyumba yao. Anatumia rangi nyeusi kumnasa Fikirini.
8. Pia wazungu wanawadhamini waafrika kwa masomo ya juu lakini waafrika wafikapo huko wanabaguliwa na kunyanyaswa.
9. Uyatima – Fikirini alimpoteza mamake akiwa kidato cha pili toka hapo inambidi ajikaze ili ajilee na awalee wengine.
10. Njaa – mwandishi anasema kuwa watu wa Afrika Mashariki wanang'ang'ana kufikisha mkono kinywani. Hivi ni kusema kuwa kuna upungufu wa chakula. Nacho chakula cha kizungu hakimkai na hivyo anaishia kuwa na njaa.
11. Umaskini - nchi za Afrika ni maskini zikilinganishwa na nchi za maghabiri. Hata hivyo Fikirini anatamani amalize masomo yake arudi kwao akafaidi utajiri wa umaskini wao.

MTAZAMO WA WAZUNGU KUHUSU WAAFRIKA NA RANGI NYEUSI KWA JUMLA

1. Waafrika hawavai nguo.
2. Kuwa kuna magonjwa mengi sana Afrika – mtu anaugua ukimwi, malaria, polio na utapia mlo.
3. Kuwa waafrika hutembea uchi.
4. Kuwa kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe.
5. Waafrika ni weusi sana - ni weusi wa kuangukiwa na lami au mionzi ya jua?
6. Afrika ni nchi si bara.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

7. Waafrika wanaishi kwa miti kama tumbiri.
8. Wasichana wote wa kiafrika wanakeketwa na kushonwa ili kuzuia ukware.
9. Afrika ni bara lenye uchawi.
10. Waafrika wakienda Marekani husumbua tu.

SIFA ZA WAHUSIKA

1. FIKIRINI

1. Ana subira/mvumilivu – anavumilia mateso na madharau anayofanyiwa huko Marekani. Mfano – kuachwa na basi, kutusiwa na Fiona, kuitiwa polisi na anavumilia baridi kali wakati akitembea shuleni na vilevile anapofukuzwa uchi na Fiona.
2. Anajiheshimu – wakati Fiona anamtaka, yeye anakataa katakata. Hapapii fursaa hiyo eti kwa sababu imetokea.
3. Mzalendo/mwenye mapenzi kwa nchi yake.
4. Japo amepata nafasi ambayo wengi wangeihusudu, anatazamia kwa hamu siku atakapomaliza masomo yake ili arudi kwao Afrika Mashariki.
5. Vyakula vya ng'ambo na maisha kwa jumla havimkai.
6. Mwenye utu/ubinadamu – haoni ni kwa nini wazungu wambague ilihali yeye ni binadamu pia. Visa vya kubaguliwa vinamkera mfano anapoachwa na basi.
7. Msomi – kwa sasa anasomea somo la uzamifu katika lugha ya kiingereza. Amepata udhaminii kutoka kwa serikali ya Marekani.
8. Anashawishika haraka – Fiona anapomwambia kuwa atampeleka chuoni anakubali kuandamana naye eti wachukue gari la Fiona
9. Anapomwona akija weusi wake unamshawishi kuwa Fiona ni mweusi mwenzake mambo yanabadilika baadaye.
10. Mlevi – amewahi kushiriki kwenye ulevi katika vitongoji duni mfano Mathare, Kenya, Ubungo Daresalaam na Kibuye Kampala.
11. Msiri – anaapa kukiweka siri kisa cha kuvulishwa nguo na Fiona. Hata kama atalewa na kileo kipi ameapa hatakifichua kisa hiki kwa yeyote.
12. Mtani – napotaniwa na wazungu kuhusu waafrika kwenda uchi anawajibu kuwa wazungu wameanza kuwaiga waaafrika hasa wakati wa kiangazi. Kuwa wakati huu wanawake wazungu huwa hawataki nguo tena; zinawakera.
13. Mnafiki – anapoambiwa na Fiona kuwa angepelekwa chuoni anajifanya hataki lakini anataka "kisebusebu na kiroho ki papo".
14. Mwoga – anapotishiwa na Fiona na Bob alimimina mkojo kwenye sakafu ya ukumbi kutokana na hofu na mishemishe.
15. Mwenye tahadhari – mwishoni mwa hadithi anakuwa na tahadhari na watu weupe, polisi na ndugu zake weusi.
16. Ana msimamo dhabiti – anakataa vishawishi vyake Fiona. Si kwamba hakuwa na pesa lakini aliona haifai.
17. Ana tamaa ya wanawake – anapomwona Fiona moyo unamtuta. Uk 25. Anakumbuka dada zake kule nyumbani- wahaya, wanyankole na wakamba.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

UMUHIMU WAKE

1. Ametumiwa kuonyesha vijana wanaofanya juhudi katika masomo – anapopewa udhamini kwenda Marekani kwa sababu ya juhudi zake za kimasomo.
2. Kuonyesha namna wazungu wanawabagua watu weusi. Anapatwa na masaibu teletele kwa sababu ya weusi wake.
3. Ametumiwa kuonyesha maafa yanayowakumba waaafrika wanaoenda ulaya kwa masomo ya juu.
4. Ametumiwa kuonyesha ulinganuzi wa hali ya maisha katika Afrika mashariki na Marekani mf. Hali ya anga, undugu nk.
5. Ametumiwa kuonyesha sifa za wahusika wengine mfano Fiona.
6. Ametumiwa kuonyesha jinsi ulevi umeenea katika Afrika Mashariki kwa kila eneo la Afrika Mashariki analoenda kuna vileo haramu mf. Waragi, gongo na chang'aa.
7. Ametumiwa kuonyesha ukatili wanaopitia waafrika mikononi mwa wazungu mfano kuvulishwa nguo, kufukuzwa uchi, kutishwa nk.
8. Anaonyeshwa kuwa waafrika wanaenda ng'ambo wasipojiheshimu na kuwa na msimamo dhabiti basi huenda wasiyafikie malengo yao. Analenga tu elimu licha ya kuwa ana masaibu mengi. Anatamani siku atakapomaliza ili arudi kwao.

2. FIONA

1. Katili – anamwambia Bob ampige risasi Fikirini.
   - Anamwamrisha Fikirini kuvua nguo licha ya baridi kali iliyoko.
   - Anatisha kumkata nyeti na kisu.
2. Mkware/kahaba/mzinzi – anamtaka Fikirini kimapenzi kwa malipo
   - Hajali kiasi atakachopewa na Fikirini mradi wana makubaliano.
   - Anamwuliza Fikirini ana pesa ngapi.
3. Mnafiki anajifanya mzuri kwa Fikirini kuwa angempeleka chuo kumbe alitaka kufanya mapenzi naye apate pesa.
   - Anamwambia Fikirini kuwa yeye ndugu yake lakini anaishia kumvulisha nguo na kuamrisha apigwe risasi.
4. Mwongo – anamwita Bob haraka haraka kwa madai kuwa Fikirini anataka kumbaka ukweli ni kuwa yeye ndiye aliyetaka kumbaka Fikirini.
   - Anamwambia Fikirini atampeleka chuoni japo hizi zilikuwa hila zake. Hakumpeleka. Aliishia kutaka kufanya mapenzi naye na kumtishia maisha.
5. Mchafu – nyumba yao ni chafu. Maguo machafu yametapakazwa kiholela na makochi yana utando wa vumbi.
6. Kigeugeu – anapoona kuwa Fikirini hamtimizii haja zake, anabadilika mara moja. Anakuwa katili na hata kumtishia maisha.
7. Makubaliano yake na Fikirini yalikuwa kuwa angempeleka chuoni lakini pindi tu Firikini anapoingia kwake, anabadilisha lengo.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

8. Mwizi/mnyang'angi/jambazi – anamwibia Fikirini pesa zake zote. Isitoshe pia anamnyang'anya kadi zake za simu na za benki, vitabu, kalamu nk..
9. Mbaguzi – anambagua Fikirini kwa misingi ya asili yake. Hawathamini waafrika anaona kuwa waafrika wanaenda Marekani kuwaharibia maisha yao na starehe zao.
10. Mwenye vitisho – anamwambia Fikirini avue nguo au….
    Anamshikia Fikirini kisu na kumwekea ubavuni.
11. Mkali – Fikirini anapokataa mambo yake, Fiona anamwita Bob kwa ukali na sura yake inabadilika ghafla na kuwa na ukali.

UMUHIMU WAKE

1. Anatumika kuonyesha ufuska ambao huendelea katika nchi hizi za kimagharibi. Anamtaka Fikirini kimapenzi licha ya kuwa nduguye Bob yuko katika nyumba iyo hiyo.
2. Uchafu wa nyumba yake unaonyesha uchafu wa tabia zake. Nyumba imejaa vumbi, nguo chafu na makochi yana utando wa vumbi. Fikirini anaiona hali hii kama fujo.
3. Yeye mwenyewe haoni haya kumtaka Fikirini kimapenzi kwa malipo. Pia anamfukuza uchi.
4. Anaonyesha jinsi ubaguzi wa rangi unavyoshika mizizi katika nchi za kimagharibi – waafrika hawatakikani huko na wanaonekana kama ambao wanaenda huko kusumbua. Hakushtakiwa japo anaendeleza ukatili huu. Fikirini anashtakiwa kwa makosa madogodogo.
5. Ni kielelezo cha ukatili unaendelezwa dhidi ya waafrika – kuwatishia kwa kisu, risasi, kuwavulisha nguo, kuwaibia.
6. Aonyesha kuwa wamarekani weusi wanaishi kwa hali ya umaskini. Wao huishi kwa nyumba na hali duni.

3. BOB

1. Ni jambazi sugu – anashirikiana na dadake kuwaibia waafrika wageni.
2. Mbaguzi – hataki akina Fikirini kule Marekani. Hataki kuitwa ndugu na Fikirini.
3. Mwenye hadhari - hataki dadake amuue Firikiri eti maafa yangezuka wakati huo.
4. Amekosa maadili – ana shughuli za ujambazi ambazo anatenda kwa ushirikiano na dadake.

Angalia wahusika hawa

1. Wanafunzi chuoni
2. Dereva wa basi
3. Mteja mzungu aliyeita polisi.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

MBINU ZA LUGHA

TASWIRA

1. Hali ya anga inatupatia taswira kamili kuhusu jinsi mambo huwa wakati wa baridi. Kila kitu ni cheupe kwa sababu kimefunikwa na blanketi kubwa la theluji.
2. Umbo la Fiona – mwandishi anasema alikuwa jimama lililofungasha si haba uk 26.
   Uk 25 – mwandishi anasema kuwa alikuwa pandikizi la jimama limekula likashiba hapa anatupatia taswira ya ukubwa wa Fiona.
3. Uk 24 – taswira ya polisi wa 911 wamemzingira Fikirani na kumwelekeza bastola. Magari yao yakimetamesha taa za dharura.
4. Chumba cha Fiona na Bob
   Uk 26 – makochi yana utando wa vumbi, maguo machafu yametapakazwa kiholela sakafuni, vumbi limetapakaa kwenye kochi aliloambiwa akalie, taswira hii inadhihirisha uchafu wao.
5. Uk 29 – Fikirini akikimbia tuputupu kama alivyozaliwa.
6. Ulevi unaotumika kule Afrika Mashariki unaleta taswira ya umaskini. Watu hulewa chang'aa, waragi, na gongo. Ajabu ni kuwa hata wale ambao wamesoma kama Fikirini wanashiriki katika ulevi huu.

MBINU REJESHI

1. Uk 22 – wakati Fikirini anaachwa na basi na hivyo kuamua kutembea, ananyapinyapia nyapunyapu na kupepesuka pepesu pepesu, kama mlevi chakari. Katika hali hii alikumbuka siku zake za fahari alipofuatia waragi kwenye kitongoji duni cha kibuye, Kampala, gongo kwenye vichochoro vya ubungo Daresalaam na chang'aa kwenye fondogoo la Mathare, Nairobi.
2. Uk 22 – taswira ya ubaguzi inapomwingia akirini, anafikiria kuhusu kudhalilishwa kwa mtu mweusi. Papo hapo anakumbuka maneno ya Rais Moi "msifikiri kwamba mzungu anatupenda sisi watu weusi" siku hizo hazikuwa na maana lakini kwa sasa anapobaguliwa basi maneno haya yana maana.
3. Uk 23 – anapotamani nyumbani kwao na kufafanukiwa kuwa "nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni", anakumbuka mara ya kwanza alipojikuta darasani yeye peke yake mtu mweusi na jinsi mhadhiri mweupe na wanafunzi weupe walivyomsaili maswali ya kumdhalilisha na kumdunisha kwa kumwuliza maswali ya kijinga.
4. Uk 24 – inapomdhihirikia kuwa jela imeundiwa mtu mweusi, kuwa wanaume weusi wanakula kalenda kuliko kusoma, anakumbuka jinsi yeye mwenyewe alivyoepuka jela kimungumungu. Alienda mkahawani na kuagiza chakula. Baada ya kula akaingia msalani lakini akasahau kufunga zipu. Ndipo mwanamke mmoja mweupe alipopiga simu kwa polisi. Lakini alipopelekwa mahakamani jaji mweusi alimpiga tu faini ya dola 200.
5. Uk 25- Fikirini anapomwona Fiona, anawakumbuka dada zake kule nyumbani Afrika Mashariki – wahaya aliokutana nao alipokuwa anasomea ualimu katika

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

chuo cha walimu cha Mwanza. Wanyankole aliokutana nao alipowahi kuzuru Uganda Magharibi na wakamba aliokutana nao alipokwenda ziara Kitui.

6. Uk 29 – Fiona anapomwamrisha Bob ampige risasi Fikirini, Fikirini anamsihi Bob asimpige risasi huku akilia machozi kama mtoto mdogo, katika hali hii Fikirini alikumbuka siku ya mamake mzazi kufa huko kwao Afrika. Fikirini alikuwa katika kidato cha pili. Hakulia wakati huo lakini alijipata akilia mikononi mwa Bob na Fiona.

MISEMO

1. Likija basi lingine ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe uk 22.
2. ..umetokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua uk 23.
3. Sharti ajipende yeye mwenyewe, ajienzi, ajionee fahari uk 23.
4. Mara mbili ametozwa faini na polisi uk. 23.
5. …wanang'ang'ana kula kalenda uk 24.
6. …aliona amekaziwa macho vibaya uk 24. Kufumba na kufumbua, polisi .. uk 24.
7. Moyo ulikuwa ukimtweta kwa fadhaa uk 24.
8. Alikuwa hata hajajibu alipopigwa pingu mikononi. Uk 24.
9. Mtu angefanya hisani ya kumwambia uk 24.
10. Fikirini alipopiga darubini nyuma hakuwa na budi… uk 24.
11. ….vinginevyo kisomo chake cha juu kingegonga ukuta. Uk 25
12. Kwa desturi Fikirini huvaa tabasamu uk 25.
13. Moyo ulimtuta uk 25.
14. …huona fedheha kuwasabahi ndugu zao weusi uk 25.
15. Fikirini alisema kwa roho ya kisebusebu na kijoyo ki papo uk 23.
16. …alijikuta amesakimu amri na anarudi nyuma uk 26
17. Maji yamezidi unga uk 26
18. Akajua dunia hii haimweki tena uk 27.
19. Mimi namkata na liwe liwalo uk 29.
20. We utazua zani hapa uk 29.
21. …kuanza kuhisi vyanda vyake vinakufa ganzi uk 29.

TASHBIHI

1. Alinyapia nyapunyapu na kupepesuka pepesupepesu kama mlevi chakari uk 23.
2. Weupe wa theluji umehanikiza na kufunika kila kitu kama blanketi uk 23.
3. Je, mwaishije kwenye miti kama tumbiri? Uk 23.
4. ..kumwona yule mama mzungu kama hasidi aliyemwitia polisi uk 24.
5. Mweusi mwingine aliyekuwa kama kisiwa kwenye bahari ya weupe uk 25.
6. …akitetemeka kama majani ya mgomba kwenye dhoruba uk 27.
7. Fikirini alihisi huku akilia machozi kama mtoto mdogo uk 29.
8. Alijitosa nje tuputupu kama alivyozaliwa uk 29.
9. Hakuhisi mzizimo wa theluji iliyokuwa inaanguka kama matone ya mvua ya mawe. Uk 29.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

10. Mambo mengine yanakuwa kama ndoto uk 30.
11. …kukimbia kasi na tuputupu kama mtu aliyepagawa pepo mbaya.
12. Zilikuwa zimeshika baridi na kuzizima kama mwili wake ulivyozizima.

TABAINI

i) Anatumia tabaini kusistiza kuhusu wingi wa barafu.
..si madirisha, si milango, si paa si kuta, si majani ya miti..

TAKRIRI

1. Uk 22 – theluji na barafu kila mahali. Kila mahali barafu na theluji.
2. Uk 22… sharti mtu avae safu ya maguo na maguo na soksi nzito pamoja na viatu, viatu vizito.
3. Uk 23 nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni.
4. Uk 24 mkahawani alikumbana na mitazamo ya dharau…au mitazamo hiyo haikumshtua.
5. Uk 25 naam wamarekani weusi, ndugu zake weusi…
6. Uk 25 – mweusi mwenzake. mweusi mwingine alikuwa kama kisiwa kwenye bahari ya weupe, weupe wa mazingira na weupe wa watu.
7. Uk 30 hasadiki kama bado yuko hai. Hasadiki kama yote…
8. Uk 30 " sasa kaazimia hutahadhari na watu weupe, polisi na ndugu zake weusi. Sasa lazima ajihadhari na ndugu zake weusi.
9. Uk 29-30 mwandishi anatumia takriri kuonyesha kuwa Fikirini alibaki bila chochote baada ya Fiona kumchakura.
   Hana vitabu, hana mkoba wa vitabu, hana pochi, hana vitambulisho, hana makadi yake mbalimbali.
10. Uk 29 alijitosa nje tuputupu.

METHALI

1. Uk 23 – nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni – Fikirini alikuwa akitamani nyumbani. Hii ni baada ya kukumbuka siku yake ya kwanza alipojikuta mweusi peke yake darasani.
2. Uk 24 – simba akikosa nyama hula nyasi – Fikirini alibidika kula chakula cha Marekani. Si kitamu kama cha kwao.
3. Uk 24 – baharia wa pemba kufa maji mazoea. Fikirini alizoea kutazamwa vibaya/kudharauliwa.
4. Uk 29 – siku ya kufa kwa nyani miti yote huteleza – yaani mambo yakianza kuharibika, hata mtu afanye nini hakuna linalotengenea.

KINAYA

1. Ni kinaya kuwa wamarekani weusi wanawabagua waafrika kwa misingi ya asili yao (Afrika) ilihali wao wenyewe wana asili yao katika Afrika yenyewe.
2. Ni kinaya kuwa wamarekani wako mstari wa mbele kushinikiza mataifa ya Afrika kuhusu utekelezaji wa haki za kibinadamu ilihali Fikirini aendapo huko haki zake za kibinadamu zinavunjwa.
3. Polisi nchini Marekani wana jukumu kubwa sana la kulinda usalama. Hata hivyo wanamdhalilisha Fikirini.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG

4. Elimu ya Marekani ni ya kiwango cha juu. Hata hivyo kuna wamarekani ambao wanatumikia vifungo kuliko kusoma.
5. Uk 24 – Fikirini anafikiria kuwa yule mama mweupe anapiga simu kwa sababu kasonona na mpenziwe au ameolewa na ndoa yake inaelekea kusambaratika. Kumbe alikuwa akiwapigia polisi simu kwa sababu ya Fikirini.
6. Uk 24 – ni kinaya kwa polisi kumwuliza Fikirini iwapo anazungumza kiingereza. Yeye ni mwanafunzi wa uzamifu katika somo la kiingerza na labda hata anajua kiingereza kuliko askari hawa.
7. Uk 25 – Fikirini anafurahia sana anapomwona Fiona. Anamfikiria kuwa mweusi mwenzake. Baadaye Fiona anageuka kuwa jambazi na hata kuyahatarisha maisha ya Fikirini.
8. Ni kinaya kuwa wamarekani weupe wanawabagua wamarekani weusi ilhali wote ni wamarekani ambao wako na haki sawa kama wananchi.
9. Ni kinaya kuwa Fikirini anabaguliwa na wamarekani ilhali serikali yenyewe imempa udhamini. Walimpa udhamini ili wakambague? Wao ndio waliomwita.
10. Uk 23 – ni kinaya kuwa wazungu wanawacheka waafrika kuwa hawavai nguo ilhali wazungu wenyewe (wanawake) hawataki nguo hasa wakati wa kiangazi.

HTTP://ATIKASCHOOL.ORG